22122841

International Baccalaureate®
Baccalauréat International
Bachillerato Internacional

**SWAHILI *AB INITIO* – STANDARD LEVEL – PAPER 1**
**SWAHILI *AB INITIO* – NIVEAU MOYEN – ÉPREUVE 1**
**SWAHILI *AB INITIO* – NIVEL MEDIO – PRUEBA 1**

Monday 14 May 2012 (afternoon)
Lundi 14 mai 2012 (après-midi)
Lunes 14 de mayo de 2012 (tarde)

1 h 30 m

---

TEXT BOOKLET – INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not open this booklet until instructed to do so.
- This booklet contains all of the texts required for Paper 1.
- Answer the questions in the Question and Answer Booklet provided.

LIVRET DE TEXTES – INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- N'ouvrez pas ce livret avant d'y être autorisé(e).
- Ce livret contient tous les textes nécessaires à l'Épreuve 1.
- Répondez à toutes les questions dans le livret de questions et réponses fourni.

CUADERNO DE TEXTOS – INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No abra este cuaderno hasta que se lo autoricen.
- Este cuaderno contiene todos los textos para la Prueba 1.
- Conteste todas las preguntas en el cuaderno de preguntas y respuestas.




© International Baccalaureate Organization 2012

https://xtremepape.rs/

**KIFUNGU A**

# NDOTO YANGU: KUWA MWANARIADHA MAARUFU



"Napenda kukimbia kwa sababu nikikimbia nakuwa na nguvu, na mwili wangu hauwezi kushambuliwa na magonjwa mbalimbali," ndivyo anavyoanza kwa kusema kijana Jamal Athuman Yusuf ambaye ameonyesha uwezo mkubwa katika riadha.

Kijana huyu anaishi Yombo, Vituka, jijini Dar es Salaam, na anaonekana kuwa na tabia ya kujituma hata anapokuwa anacheza na wenzake.

Jamal anasema anapenda sana kukimbia kwa sababu kwa kukimbia mwili wake umekuwa mwepesi. Anasema amekuwa akishindana viwanjani na watoto wa shuleni na rafiki zake mtaani kwao kwenye mchanga, na amekuwa akishinda mbio hizo zote.

Anasema kwa sasa ndio ameanza kidato cha kwanza katika shule ya sekondari, na kwamba matumaini yake ni kuendeleza kipaji (*talent*) chake cha kukimbia. Jamal anaendelea kusema kuwa atakapoendeleza kipaji chake ataitangaza nchi yake kwa kupitia mchezo huo wa kukimbia, na yeye atakuwa maarufu na atakuwa na pesa nyingi.

*Habari Leo Jumapili* (2011)



https://xtremepape.rs/

**KIFUNGU B**

# VIJANA WAZUNGUMZIA AINA YA VYAKULA WANAVYOVIPENDA

***Hayo hapo chini ni mawazo ya wanafunzi kuhusu aina za vyakula wanavyovipenda.***

Naitwa Mustapha Ramadhani. Mimi napenda chipsi na kuku kwa sababu ni chakula kizuri. Lakini nyumbani mama akipika chakula kingine mimi nakula kwa sababu kuku ni ghali sana kuliko maharage. Chakula chochote mimi nakula nyumbani.





Naitwa Samira Hamza. Mimi ninapenda wali na maharage kwa sababu ni chakula kitamu. Halafu nikila wali na maharage nitakuwa mkubwa, mwenye nguvu nyingi kama simba. Lakini mama akipika chakula kingine mimi sikatai, ninakula.

Ninaitwa Olivia Stanford. Mimi ninapenda chakula gani unajua? Ninapenda kula pilau. Ninapenda kula pilau kwa sababu ni chakula kizuri, halafu hakiliwi mara kwa mara kama chakula kingine. Ni chakula cha sikukuu. Lakini mama akipika chakula kingine ninakula.





Naitwa Sarafina Christopher. Mimi napenda chipsi na mayai kwa sababu ni tamu. Kama tukienda kutembea na mama na baba, nikichoka wananinunulia chipsi na mayai. Lakini nyumbani wakipika chakula kingine ninakula kwa sababu sitaki kumkasirisha mama yangu. Anapokasirika ninasikitika. Nampenda sana.

*Habari Leo Jumapili* (2011)



https://xtremepape.rs/

**KIFUNGU C**

# KALENDA YA KENYA NA TANZANIA

## KENYA

**JULAI**

**Tamasha (festival) la *Storymoja***

Tamasha hili litafanyika katika ukumbi wa Impala, Nairobi. Ni tamasha la kusimulia hadithi mbalimbali za Kenya, Afrika ya Mashariki, na hata nje ya Afrika ya Mashariki.

**AGOSTI**

**Tamasha la Fasihi la Kwani**

Tamasha la fasihi lina matukio mengi zaidi ya fasihi. Hapa kuna warsha za namna ya kuandika vitabu vya fasihi, mihadhara, maonyesho ya vitabu na usomaji wa vitabu katika sehemu mbalimbali za Nairobi. Waandishi wa vitabu, waandishi wa habari na wachapishaji wa vitabu wanakuja kwa wingi kutoka sehemu mbalimbali za Kenya na barani Afrika kwa ajili ya tamasha hili la kila mwaka.

**SEPTEMBA**

**Tamasha la Kimataifa la Vitabu**

Tamasha la vitabu na la kimataifa ni la kila mwaka. Linafanyikia katika ukumbi wa Sarit, jijini Nairobi. Katika tamasha kuna majadiliano, ushairi na usomaji wa vitabu, hasa vitabu vipya, unaofanywa na watu mbalimbali.

**OKTOBA**

**Tamasha la Kimataifa la Biashara**

Tamasha linafanyikia Nairobi katika viwanja vya Jamhuri Park. Linaonyesha bidhaa nyingi za biashara na kilimo cha Kenya.

## TANZANIA

**JULAI**

**Maonyesho ya Dar es Salaam ya Kimataifa ya Biashara**

Maonyesho yanafanyika tarehe 7 katika Viwanja vya Maonyesho vya Mwalimu Julius Nyerere. Maonyesho haya ni muhimu sana kwa hiyo tarehe 7 Julai ni sikukuu pia. Kunakuwa na maonyesho zaidi ya 1500 kutoka nchi zaidi ya 20 duniani.

**AGOSTI**

**Tamasha la Kimataifa la Filamu Zanzibar**

Tamasha hili la filamu ni kubwa kuliko yote Afrika ya Mashariki. Katika tamasha hili kunakuwa na watengeneza filamu wengi sana kutoka Tanzania na nje ya Tanzania – wazee na vijana. Filamu mbalimbali mpya zinaonyeshwa na kushindana. Pia kunakuwa na wasanii, hasa wanamuziki mbalimbali, kutoka duniani kote ambao wanafanya maonyesho ya muziki wao.

**SEPTEMBA**

**Sherehe ya Mwakakogwa, Zanzibar**

Sherehe hii ya kila mwaka inayofanyikia Makunduchi, Zanzibar, hutegemea kuonekana kwa mwezi. Ni sherehe inayofanyika kwa siku nne mfululizo. Ni sherehe ya kuanza kwa "mwaka mpya" wa watu wa sehemu hii. Kunakuwa na sherehe nyingi za utamaduni na shamrashamra nyingi.

**OKTOBA**

**Makua**

Sherehe hii hufanyikia Mtwara, Kusini mwa Tanzania. Kunakuwa na ngoma na maonyesho ya sanaa mbalimbali za makabila ya Wamakonde, Wamakua na Wayao kutoka sehemu hizi.

*Paa* (2010)



https://xtremepape.rs/

**KIFUNGU D**

# LIKIZO! LIKIZO!

Je wewe ni mwanafunzi na unakaribia kupata likizo? Basi huu ni wakati mzuri kwa sababu tumemaliza mitihani. Unataka kwenda mahali pa ndoto zako? Twende Ziwa Victoria katika jiji la Mwanza, Tanzania. Je unajua kuwa Ziwa Victoria ni la pili kwa ukubwa duniani?

Ziwa Victoria ni ziwa kubwa kuliko yote barani Afrika. Pia ziwa hilo linafahamika kwa jina la Ziwa Nyanza. Linashikilia namba ya pili kwa ukubwa duniani. Ziwa la kwanza kwa ukubwa duniani ni ziwa la Superior ambalo lipo Marekani ya Kaskazini.

Ziwa Victoria lipo futi 3,726 kutoka usawa wa bahari, na lina eneo la maili za mraba zaidi ya 26,000. Maji ya Ziwa Victoria, ambayo si ya chumvi, yanamiminika kwenye mto Nile na kuelekea bahari ya Mediterranean kwa umbali wa maili 4,000.



## MIPANGO YA LIKIZO

Tutaondoka Dar es Salaam na wengine watatoka Moshi, Nairobi na sehemu nyingine. Tutakutana katika jiji la Mwanza, linalojulikana kama *Rock City*, tarehe 15 Julai. Tutakaa hoteli ya *Tai Five*. Hapo tutapanga ratiba yetu vizuri, lakini tukiwa huko tutaogelea katika ziwa, tutavua samaki, tutaenda disco jijini Mwanza, na tutatembelea Chuo Kikuu cha SAUT. Ni vizuri wote mtumie mabasi ili muone mazingira njiani, hasa ya milima, mito, mashamba ya watu na hata mbuga za wanyama. Pia kusafiri kwa basi si ghali kama kwa ndege.

Wanaotaka kujiunga nasi wapige simu namba +255 789 377 517
au barua pepe: femk.coded@gmail.com.

*Msafiri*, Edition 71 (2010) na *Habari Leo Jumapili* (2011)



https://xtremepape.rs/